


KUTOLEWA KWA MARA MOJA: Aprili 23, 2020

# Gavana Whitmer na Taasisi za Fedha za Michigan Wamekubaliana Kushirikiana Kutoa Malipo ya Uvumilivu ya Rehani kwa Wakopaji kwa siku 90

Gavana Gretchen Whitmer na Idara ya Huduma za Bima na Huduma za Fedha ya Michigan (DIFS) leo wametangaza kuunda Ushirikiano wa Msaada wa ***Ushirkiano Nafuuu Wa Rehani*** pamoja na zaidi ya taasisi 200 za kifedha za Michigan kutambua na kupanua hatua ambazo taasisi hizi zimekuwa zikichukua kuwasaidia wateja ili kuhakikisha ya kuwa hakuna mtu anayepata shida ya kifedha kwa sababu ya COVID-19 watapoteza nyumba zao wakati huu wa shida kwa afya ya umma.

Taasisi za kifedha za Michigan zimekuwa zikifanya bidii kuwasaidia wateja wao wakati huu usio wa kawaida. Ushirikiano huu utahimiza usawa katika chaguzi zinazopotikana kwa wateja wanaohitaji msaada, bila kujali taasisi ya kifedha.

“Hakuna mtu anayepaswa kuwa na wasiwasi kuhusu kupoteza nyumba yao wakati wa mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19,” Gavana Gretchen Whitmer alisema. “Pamoja na Ushirikiano wa ***Ushirkiano Nafuuu Wa Rehani,*** mashirika ya umoja wa mikopo ya Michigan, benki, na wakopeshaji wamejitokeza kuwasaidia wakazi wetu ambao wana shida ya kifedha kutokana na COVID-19 kwa kutoa kipindi cha neema cha siku 90 cha malipo ya rehani.

Kwa kusaini kwa Gavana Whitmer kwa ***Ushirkiano wa unafuuu Wa Rehani*** ushirikiano kwa taasisi za kifedha umekubaliana kuendelea kuwasiliana na wakaaji wao walioathirika na angalau kwa njia zifuatazo:

**Kuwapa wakopaji walioathirika kipindi cha neema cha siku 90 kwa malipo yote ya rehani.** Taasisi za kifedha zitatoa uvumilivu wa malipo ya rehani kwa siku 90, kuruhusu wakopeshaji kupunguza au kuchelewesha malipo yao ya rehani ya kila mwezi ya rehani. Zaidi ya hayo, taasisi za kifedha zita:

- Toa mchakato ulioratibiwa na kuomba uvumilivu kwa sababu zinazohusiana na COVID-19, zilizoungwa mkono na hati zinazopatikana;
- Thibitisha idhini ya na sheria ya mpango wao wa uvumilivu (ambao unapaswa kujumuisha suluhisho sahihi za malipo ya kuanza baada ya muda wa uvumilivu); na
- Ikiwezekana, wakopaji wapewe nafasi ya upanuzi wa makubaliano ya uvumilivu ikiwa wataendelea kupata shida kutokana na COVID-19

**Kutoa unafuu kutoka kwa ada na malipo za kuchelewa inayohusiana na malipo ya rehani kwa siku 90.** Kwa wakopaji walioathirika ambao watafikia makubaliano na taasisi yao ya kifedha, taasisi za kifedha zitatoa au kuwarudisha wateja ada ya kuchelewa kutokona na malipo ya rehani kwa siku 90.

**Kutouza nyumba za wakopaji kwa siku 60.** Taasisi ya kifedha hazitaanzisha mauzo yoyote au kuwaondoa wakazi kutoka kwa nyumba yao kwa siku 60 kwa wakopaji walioathirika ambao wamefikia makubaliano ya taasisi yao ya kifedha.

**Kuepuka kuripoti habari mbaya kuhusu alama ya mkopo kwa msingi wa mkopaji kupokea msaada.** Taasisi za kifedha hazitaripoti habari mbaya kuhusu alama za mkopo kwa wakopaji walioathirika ambao watafikia makubaliano na taasisi yao ya kifedha. Taasisi za kifedha zitaripoti habari nyingine za mikopo inayoendana na Matumizi Ya Ulinzi Wa Kifedha Wa Ofisi Au Miongozo  Mingine Ya Wakala Wa Shirikisho or other .

**Kuwasiliana na wakopaji kuhusu mahitaji yao maalum au wasiwasi walionayo.** Ikiwa taasisi ya kifedha inatofautiana na vifungu hivi kwa faida ya akopaye au kushughulikia ombi fulani la akopaye, wasiwasi, au afya ya kifedha ya mtu binafsi, hii itazingatiwa kwa nia ya ushirika. Hasa, maswala yanayozunguka escrow na ushuru na malipo ya kodi ya bima yanaweza kuhitaji msaada zaidi wa mtu mmoja.

Kufikia Aprili 22, 2020 zaidi ya taasisi za kifedha 200 zilitia saini katika ushirikiano huu. Ushirkiano  wa taasisi za kifedha Taasisi shirikishi za fedha zimeorodheshwa kwenye kurasa ya ***UshirkianoTaasisi za kifedha za Unafuuu Wa Rehani.***

“Nguvu ya mfumo wetu wa kifedha itakuwa muhimu katika sababu ya  jinsi ambavyo Michigan inavyopona kiuchumi kutokana na COVID-19,” Mkurugenzi wa DIFS Anita G. Fox alisema. “Kupitia Ushirikiano wa ***Ushirkiano Wa Unafuuu Wa Rehani,*** taasisi za kifedha zitaendelea kusaidia wateja kupata suluhisho zinazofaa mahitaji yao, nakutia manani kutoa misaada kwa wale walioathiriwa zaid na shida hii. Wakazi wa Michigan wanaoweza kutimiza majukumu yao ya kifedha wanaweza kuendelea kufanya hivyo, na wale wanaohitaji msaada wataweza kuendelea kuwasiliana na taasisi zao za kifedha ili kupata unafuu.”

Wakopaji wa Michigan wanaopata shida ya kifedha kwa sababu ya COVID-19 wanahimizwa kuwasiliana moja kwa moja na taasisi zao za kifedha ili kuelewa maelezo ya chaguzi za misaada zilizoko tayari  kwa ajili yao, na kushirikiana na taasisi zao katika makubaliano yanayotumika

kwa mkopo wao. Wakopaji wanahimizwa kuwasiliana na taasisi zao za kifedha kabla mkopo wao haujakomaa. DIFS kamwe haushauri wakopaji kuacha kulipa malipo yao ya mkopo.

Tafadhali kumbuka kuwa taasisi za kifedha na watendaji wao wanakabiliwa na maswali mengi na wanaweza kupendekeza kutumia huduma mkondoni wakati zinapatikana kwa huduma ya haraka. Mikopo iliyowekwa na taasisi ya kifedha inaweza kuhudumiwa na kampuni nyingine.

Wakopeshaji amabo hutumia rehani iliyoungwa mkono na serikali wanakabiliwa na sharia za serikali ya federali. Wakopaji walio na mikopo hii wanaweza kuzuru CFPB guide to coronavirus mortgage relief options.

Kwa habari zaidi kuhusiana na unafuu wa rehani kutokana na COVID-19, angalia: www.michigan.gov/MiMortgageRelief au piga simu kupitia nambari ya bure ya DIFS kwa 877-999-6442.

###